TANGAZO LA SERIKALI NA.199 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 272)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 9(1) na (2))*

NOTISI YA KUONGEZA ENEO LA KUTOA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA
(MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI ARUSHA)
YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kuongeza Eneo la Kutoa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Arusha) ya Mwaka 2023.

Kuongezwa eneo la huduma

2. Eneo la huduma la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Arusha linaongezwa ili kujumuisha maeneo yaliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii.

Kusititisha utoaji wa huduma

3.-(1) Chombo chochote cha jamii au chombo kilichosajiliwa kabla ya kuanza kutumika kwa Notisi hii ambacho kinatoa huduma ya maji na usafi wa mazingira katika maeneo yaliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii kitasitisha kutoa huduma hizo.

(2) Haki, uwajibikaji, muda wa ajira, mali, madeni na masuala mengine yaliyotolewa au kufanywa na chombo cha jamii au chombo kingine chochote kilichosajiliwa kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira, yatakuwa chini ya

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Arusha.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| JINA LA MAMLAKA YA MAJI | ENEO LA HUDUMA LINALOONGEZWA | | |
|---|---|---|---|
| | WILAYA/ MJI MDOGO | KATA | KIJIJI/MTAA |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Arusha | Wilaya ya Longido | Namanga | Kata yote |
| | | Kimokowo | Loloibonyi, Endepesi, Eworendeke na Etilali |
| | Wilaya ya Simanjiro/Mji Mdogo wa Mererani | Mererani | Tunduru, Msikitini, Mirerani, Kangaroo, Songambele, Songambele A, Getini, Manyara, Kilimanjiro, Twiga, Tanzanite na Kwa Nyiti. |
| | | Endiamtu | Mji Mpya, Zaire, Tupendani, Kisimani, Cairo,Kazamoyo, Kazamoyo juu, Tenki la Maji, Endiamtu, Sekondari, Kilimahewa na Tanesco |
| | | Shambarai | Shambarai, Kandasikira |
| | | Naisinyai | Naisinyai |

Dodoma,
8 Machi, 2023

JUMAA H. AWESO
*Waziri wa Maji*